# HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

**MKOA WA RUKWA**:
FAX: 025 283 0136
SIMU: 025 283 0006
Email: ded@nkasidc.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:
*Kumb.Na.NKS/DC/ M.30/I/VOL. I/80*

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P. 2,
**NAMANYERE - NKASI.**

*Tarehe*: 01/06/2023

## MABADILIKO YA TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi alitangaza nafasi za kazi za Watendaji wa Kijiji III nafasi 03 kupitia tangazo lenye Kumb. Na NKS/DC/ M.30/I/VOL. I/80 la tarehe 03.04.2023 baada ya kupokea kibali cha Ajira Mpya kwa mwaka 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi amepokea maelekezo kutoka kwa Katibu Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuwa, kwa mujibu wa kanuni Na. 22 (1-2) ya kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti ya Ajira kama ilivyorekebishwa kupitia gazeti la Serikali Na. 580 la 2022 kuwa inaelekeza **kutumika kwa KANZIDATA** ya waliofaulu Usaili na hawakupangiwa vituo vya kazi pale inapotokea fursa ya Ajira.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilitangaza nafasi 12 mwaka wa Fedha 2021/2022 na kufanya Usaili ambapo wasailiwa wengi walifaulu na kwa kuwa nafasi zilikuwa chache hawakupangiwa vituo vya kazi.

**Hivyo, wasailiwa hao waliofaulu na kukosa fursa ya kuajiriwa wataitwa kujaza nafasi 03 zilizotangazwa**.

Kwa maelezo haya ninasitisha maombi ya nafasi za Ajira ya Watendaji wa Vijiji zilizotangazwa kwa tarehe tajwa hapo juu.

Naomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Mwakalambile, W
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**NKASI**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
NKASI